



Ajenda ya utetezi ya watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza Tanzania



 **MAONI
YETU,
SAUTI
YETU**
An initiative by the NCD Alliance
and people living with NCDs

 **NCD Alliance**

 **TANCDATA** Tanzania
NCD
Alliance

Shukrani

Ajenda ya Utetezi ya Watu Wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza nchini Tanzania ilitengenezwa kufuatia mpango anzilishi wa "Maoni Yetu, Sauti Zetu" wenye dhumuni la kuhamasisha uhusika wa kina wa watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza katika kupambana na magonjwa hayo. Juhudi za mashauriano za kuzalisha Ajenda ya Utetezi ya Tanzania ya Watu Wanaoishi na Magonjwa Yasiokuwa yakuambukiza ziliungwa mkono na Muungano wa NCD kama sehemu ya ushirikiano wake na The Leona M. na Harry B. Helmsley Charitable Trust.

Shukrani kwa wanachama wa TANCDA, watoa huduma wa kliniki zinazoshughulikia watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali ya Mkoa wa Dodoma, Hospitali ya Mkoa wa Morogoro, Hospitali ya Shree Hindu Mandal ambao waliwezesha juhudi za kufanya mahojiano. Shukrani za pekee kwa watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza ambao walishiriki kwa hiari kutoa maoni yao na mapendekezo kujenga ajenda hii ya watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza pia kuridhia picha zao zitumike katika ajenda hii

Shukrani pia ziende kwa Prof Andrew Swai, Prof Kaushik Ramaiya, Dk Tatizo Waane, Happy Nchimbi, Elizabeth Licoco na Vivid Maimu wa TANCDA ambao walishiriki kuongoza juhudi za kufanya mahojiano na watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza na ndugu zao/walezi.

Rasimu ya kwanza ya Ajenda ya Utetezi ya Watu Wanaoishi na magonjwa yasiyoyakuambukiza nchini Tanzania ilipitiwa na wanachama wa TANCDA (Hilda Missano, Dr George Msengi na Roman Mathias), Watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza (Mr Ramadhani Mongi, Ms Arafa Saidi, Ms Neema Mohamed na Norbert Silayo) na wadau wengine kabla ya kukamilika. Pia imepitiwa na kupokea maoni kutoka kwa Bi Manjusha Chatterjee na Bi Katrina Barker wa shirikisho la vyama vya magonjwa yasiyoambukiza duniani (NCD Alliance)

Imehaririwa na Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza (TANCDA)
Hakimiliki © 2021 Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza (TANCDA) Alliance
Imechapishwa Dar es Salaam, Tanzania

Picha zote zilipigwa wakati wa vikao vya majadiliano na watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza katika mikoa ya Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam

Picha: TANCDA
Ubunifu na mpangilio: Mar Nieto
Imetolewa mwaka 2021

Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza (TANCDA) Alliance
Hospitali ya Taifa Muhimbili
Eneo la makuti Makuti B
Karibu na klinik ya kisukari
S.LP 65201
Dar es Salaam
Tanzania
www.tancdatz.or.tz

Yaliyomo

Sisi ni watazania tunaishi na magonjwa yasiyoambukiza Sauti zetu ni muhimu zisikike na maoni yatekelezwe kwa vitendo	5
Utangulizi	6
Uandaaji wa Ajenda hii ya Utetezi	8
Haki za Binadamu na Haki za Kijamii	10
Kuzuia	11
Matibabu, Matunzo Na Msaada	12
Meaningful Involvement	14





Sisi ni watanzania tunaishi na magonjwa yasiyoambukiza Sauti zetu ni muhimu zisikike na maoni yatekelezwe kwa vitendo

Sisi sote tupo hatarini kupata magonjwa yasiyoambukiza bila ya kujali umri, jinsia au hali ya kijamii na kiuchumi.

Magonjwa yasiyoambukiza yanatuathiri kimwili, kiakili, kihisia, kijamii na kiuchumi na maelfu ya Watanzania wanapoteza maisha yao kwa sababu ya magonjwa yasiyoambukiza kila mwaka. Tumekuwa na changamoto ya gharama kubwa za matibabu na dawa, kucheleweshwa kwa utambuzi, ukosefu wa huduma za ushauri na gharama kubwa za kusafiri kwenda kwenye vituo vya afya. Tunakumbana na unyanyapaa katika maisha yetu kazini, shuleni na katika jamii. Magonjwa yasiyoambukiza yanaweza kuzuilika na juhudi zinapaswa kufanywa ili kuepusha mateso yatoakanayo na magonjwa haya

Sisi, Watu tunaishi na magonjwa yasiyoambukiza tunaamini hatujahusishwa ipasavyo katika majadiliano juu ya afya zetu.

Sisi tumeungana pamoja kama watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza kupaza sauti zetu na kuomba haki zetu juu ya kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza, matibabu stahiki na huduma ya kujimudu ambazo zinapatikana kwa bei nafuu na kwa wakati stahiki kwa wote.

Sisi ni watu ambao tuna haki, mahitaji, matumaini, majukumu na matarajio.

Sisi tunaujuzi na uzoefu wa hali zetu.

Tunatoa wito kwa wadau wote kuona umuhimu wa kutuhusisha ipasavyo sisi tunaishi na magonjwa yasiyoambukiza.

Pia tunatoa wito kwa serikali, viongozi na jamii kutambua uzoefu wetu wa kuishi na magonjwa yasiyoambukiza kama kichocheo muhimu cha kufanya mabadiliko ya sera na afua kwa wananchi.

Ili kubadilisha maisha yetu, tunapendekeza kuwa sehemu ya hatua za maamuzi na mawasiliano katika ngazi zote ikiwemo jamii na kuhakikisha kuwa maoni na sauti zetu zinasikika

Kupitia Ajenda hii, tunataka kutoa hamasa kwa wale ambao wamepoteza matumaini na wanafikiri wako peke yao katika mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza

Sisi ni wapaza Sauti za mabadiliko, kwa jamii zenye afya na taifa lenye afya!

Tunatoa wito kwa wadau kama Serikali, taasisi za kijamii, vyombo vya umoja wa mataifa, mashirika ya kimataifa, taasisi za kidini na jamii kwa hatua stahiki.

**Kwa pamoja tuna nguvu
Hii ndio Ajenda yetu ya Utetezi**

Utangulizi

Magonjwa yasiyoambukiza ni sababu kubwa ya vifo na ulemavu Ulimwenguni kote, ikichangia asilimia 71 ya vifo vyote. Magonjwa yasiyoambukiza ni tatizo nchini Tanzania na yanasababisha idadi kubwa ya magonjwa na vifo.

Kuna ushahidi wa kuongezeka kwa magonjwa yasiyoambukiza hasa katika nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania (Mayige, et al., 2012). Magonjwa yasiyoambukiza yanasababisha vifo milioni 41 kwa mwaka na zaidi ya 80% vinatokea katika nchi zinazoendelea (Shemdoe et al., 2012) na ongezeko kubwa zaidi la vifo vinavyotokana na magonjwa wasiyoambukiza duniani katika muongo ujao vinatarajiwa kutokea barani Afrika ambapo, magonjwa wasiyoambukiza yatakuwa chanzo kikuu cha vifo kufikia 2030 (Nundy na Han, 2012).

Utafiti pia unaonyesha kuwa Tanzania Bara kati ya 1994 na 2002 imepata ongezeko kutoka 15% hadi 28% ya vifo vya watu wazima vinavyohusishwa na

magonjwa yasiyoambukiza au majeruhi (Shamdoe et al., 2012). Utafiti wa Mayige (2016) unaripti kuwa makadirio ya nchi yalionyesha kuwa magonjwa yasiyoambukiza yalichangia asilimia 31 ya vifo vyote mwaka 2012.

Mpango mkakati wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2016) uliripoti kuwa magonjwa yasiyoambukiza yanachangia takriban theluthi moja ya vifo vyote nchini na ni chanzo cha kuongeza ulemavu nchini Tanzania. Utafiti wa Roman et al. (2019) inakadiria, takriban 33% ya watu wote wa Tanzania wameathiriwa na magonjwa yasiyoambukiza, haswa magonjwa ya moyo, saratani, kisukari, na magonjwa sugu ya kupumua.

Magonjwa makuu katika kundi hili ni pamoja na Magonjwa ya Moyo, Magonjwa ya mfumo wa hewa, Kisukari, na Saratani. Mengine ni pamoja na afya ya akili, hemoglobinopathies, figo, meno, magonjwa ya macho, masikio, na majeraha.



Shirikisho la vyama vya Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza Tanzania (TANCD) ni asasi isiyo ya faida inayoundwa na Chama cha Kisukari Tanzania (TDA), Taasisi ya Moyo Tanzania (HFT), chama cha Magonjwa ya mfumo wa Kupumua (TARD), Chama cha Saratani Tanzania (TCA), chama cha magonjwa ya selimundu, Chama cha Magonjwa ya Figo, Jukwaa la Kudhibiti Matumizi Tumbaku Tanzania (TTCF), Mtandao wa Kudhibiti Matumizi ya Pombe Tanzania (TAAnet), Chama cha Lishe, Chama cha Shughuli za Kimwili na mazoezi Tanzania), na chama cha wahariri na waandishi wa habari kwa madhumuni ya kukinga na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza (Magonjwa yasiyoyakuambukiza).

Kuenea kwa magonjwa yasiyoambukiza na mateso yanayohusiana - yanaongezeka kila siku, magonjwa yasiyoambukiza yanaweza kuzuilika au kucheleweshwa. Magonjwa haya huathiri familia na jamii kwa kufupisha maisha, kulemaza, kudhoofisha, na kuongeza unyanyapaa na ubaguzi. Mbali na mateso ya wanadamu, uchumi pia unaathirika kutokama na magonjwa yasiyoambukiza.

Kwa pamoja tunaipongeza serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuboresha mifumo ya afya na kuongeza vituo vya afya na kuwafukia wananchi. Agenda yetu tunaelekeza nguvu kuboresha na kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza, sisi, watu tunaishi na magonjwa yasiyoambukiza, tunaungana kupaza sauti na kudai haki zetu. Ili kuleta mabadiliko katika maisha ya watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza, tunapendekeza tuwe sehemu ya vyombo vya kufanya maamuzi na michakato ili maoni na sauti zetu zisikilizwe. Uwepo wetu, shauku, kujitolea, na ufahamu wetu kwa pamoja tunaungana katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza na pia kuhakikisha mahitaji na vipaumbele vya watu wanaoishi na magonjwa hayo vinatimizwa.



Uandaaji wa Ajenda hii ya Utetezi

Ajenda ya Utetezi ya Watu Wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza Tanzania imeandaliwa baada ya Mazungumzo na watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza wenye uzoefu wa kuishi na magonjwa hayo, iliyoendeshwa mnamo Julai na Agosti 2021.

Shirikisho la vyama vya magonjwa yasiyoambukiza lilileta pamoja zaidi ya watu 200 wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza, wakiwemo wenza au ndugu wanaowatunza ambao walibainisha mahitaji yao, changamoto, na vipaumbele vyao kuhusiana na kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza nchini.

Ajenda ya Utetezi Tanzania ilijengwa kupitia mazungumzo na jamii, mijadala ya vikundi na mahojiano ya kina, na kuwafikia takribani watu 213 wanaoishi na magonjwa mbalimbali yasiyoambukiza kutoka mikoa mbalimbali nchini Tanzania, ikiwemo Arusha, Dodoma, Dsm, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Mafinga, Mara, Mbeya, Morogoro, na Mtwara.

Uandaaji wa Ajenda hii ya Utetezi wa Watu Wanaoishi na Magonjwa Yasiokuwa ya Kuambukiza ulifanywa na kikundi kazi cha watu wanne wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza, kilichoitishwa na Shirikisho la vyama vya magonjwa yasiyoambukiza. Wakati wa kuandaa Ajenda ya Utetezi wa Tanzania, maoni yalipokelewa kutoka kwa wanachama wa TANCDA, watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza na shirikisho la magonjwa yasiyoambukiza duniani.

Ajenda ya Utetezi inatoa wito wa juu kuunga mkono katika ngazi za kisiasa, kiuchumi na kijamii ili kuweka mahitaji ya watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza katika vipaumbele kwenye sera na utekelezaji Tanzania.

Ajenda hii ya Utetezi wa Tanzania inaweka wazi mapendekezo ya wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza. Inatoa dira kwa juhudi za utetezi wa magonjwa yasiyoambukiza na kama hati hai inayotoa vipaumbele vya watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza. Inakusudiwa kuongoza na kuunga mkono juhudi za washikadau wakuu ili kuboresha uzuiaji na udhibiti wa magonjwa yasiyoambukiza.

Ajenda hii ya Utetezi wa Tanzania pia inatumika kuimarisha mwikitiko katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza. katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Ni jarida rejeo la kutumiwa na mashirika ya kiraia na watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza kuwahimiza wafanya maamuzi kuchukua hatua, kufikia malengo yaliyokubaliwa ya kimataifa na kitaifa ya magonjwa yasiyoambukiza pia kuweka watu mstari wa mbele. Inaweza kutumika kimkakati kulingana na mpangilio na fursa za utetezi wa magonjwa yasiyoambukiza.

Ajenda hii ya Utetezi imejikita katika maeneo makuu manne:




Haki za Binadamu na
Haki ya Jamii



Kuzuia



Matibabu, Utunzaji
na Msaada



Kuhusishwa
kikamilifu

Maeneo manne ya Ajenda ya Utetezi Tanzania ya Watu Wanaoishi na Magonjwa yasiyoambukiza yana uhusiano wa karibu, na kufikia hatua moja kunahitaji maendeleo kwa mengine yote. Haki za binadamu, haki ya kijamii, na ushiriki wa kikamilifu wa watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza ni msingi wa hatua zote. Matarajio yetu ya kupunguza wimbi la magonjwa yasiyoambukiza na hayatafikiwa bila hatua za kuzuia, na hatuwezi kufanya maendeleo bila kutoa matibabu ya kutosha, utunzaji na usaidizi.



Haki za Binadamu na Haki za Kijamii



MUHTASARI

Sisi, watu wanaoishi na Magonjwa yasiyoambukiza nchini Tanzania wakati mwingine tunakabiliana na ukiukwaji wa haki zetu za kimsingi za binadamu. Mara nyingi tunaachwa bila fursa ya kuishi katika mazingira yanayofaa kwa afya njema na ustawi. Hatuna taarifa na habari muhimu kwa usimamizi wa hali zetu.

Tunakosa huduma bora, matibabu, na kunyanyapaliwa, kwetu sisi huu ni ukiukwaji wa haki zetu za kibinadamu. Kuna imani potofu kuhusu magonjwa yasiyoambukiza katika jamii zetu na mara nyingi watu hufikiri kuwa umerogwa.

Tunahitaji kwa pamoja kusimama dhidi ya unyanyapaa na ubaguzi shuleni, katika jamii zetu, kazini, majumbani na miongoni mwa familia. Tunahitaji kuwa wajasiri. Tunaamini kwa dhati kwamba hatua kubwa ya kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza na kupunguza udhaifu ni kuhakikisha kuwa haki za binadamu na haki za kijamii za raia wote wa Tanzania zinalindwa. Tunataka kuwa wanajamii wanaoshiriki kikamilifu, tuchukuliwe kwa heshima na utu.

Sisi, tunaishi na magonjwa yasiyoyakuambukiza, tunaomba:

Kutengeneza na kusimamia sheria, sera, kanuni na miongozo inayolinda haki za watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza katika ngazi zote.

Ushiriki katika hatua za kufanya maamuzi kuhusu hali zetu.

Kuhudumiwa kwa kuzingatia heshima, utu na faragha wakati wote

Kuwezesha uanzishwaji wa shughuli za kujiongeza kipato ili kukidhi mahitaji ya msingi

Fursa ya kupata taarifa muhimu ili kusimamia hali zetu za magonjwa, huduma bora, matibabu na msaada wa kisaikolojia

Addressing discrimination in the workplace, schools, and community against those with NCDs.

“Tunapinga unyanyapaa na ubaguzi shuleni, katika jamii zetu, kazini na katika familia.”





MUHTASARI

Sisi, watu tunaishi na magonjwa yasiyoambukiza tunapendekeza kuwekeza katika mikakati ya kuzuia magonjwa yasiyoambukiza ili kulinda familia na jamii zetu dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza na kuunda jamii yenye afya ya Kitanzania.

Kuweka ushirikiano wa sekta mbalimbali inamaanisha tunafanya kazi pamoja na kushinda pamoja kama msemu usemao "tembea peke yako na ufikie haraka lakini tembea pamoja na kufika mbali". Jumuiya zetu hukabiliwa na hatari kama vile lishe isiyofaa, kutofanya mazoezi ya mwili, matumizi ya pombe na tumbaku na uuzaji wa vyakula visivyofaa katika mazingira ya shule.

Serikali inapaswa kuendelea kuongeza uelewa juu ya vihatarishi na visababishi vya magonjwa yasiyoambukiza ili watu wabadili tabia na kupunguza wimbi la magonjwa yasiyoambukiza. UVIKO-19 pia imeleta athari kubwa kwa watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza, na tunaiomba serikali kutilia mkazo juu ya tahadhari zote ili kupunguza hatari. Tunajua kwamba gharama ya kinga ni ndogo sana kuliko gharama ya matibabu na tiba na tunataka juhudi za kinga ziimarishwe ili kulinda vizazi vijavyo vya Watanzania.

Sisi, tunaishi na magonjwa yasiyoambukiza, tunaomba:

Kufanya kampeni za uhamasishaji wa umma mashuleni na kwenye jamii juu ya magonjwa yasiyoambukiza na visababishi vyake, kwa kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii

Kuimarisha na kuzuia magonjwa yasiyoambukiza kwa kuanza na utoaji wa taarifa na machapisho mashuleni na vyuoni ambazo zitapelekea ujumuishwaji wa magonjwa yasiyoambukiza katika mitaala.

Kupitisha kanuni katika ngazi ya jamii kuhakikisha upatikanaji na unafuu wa vyakula vyenye ubora wa kilishe katika mazingira ya shule.

Kuimarisha usimamizi wa kanuni zinazodhibiti uhamasishaji, utangazaji, uuzaji, bei na kodi ya tumbaku, vileo, vyakula na vinywaji hatarishi.

Kurekebisha sera ya kitaifa ya afya na kanuni zinazohusiana ili kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza

Kuwepo na mpango mkakati wa maendeleo ya miundombinu ili kuhamasisha na kuboresha mazoezi ya mwili kwa wote.

Kuwa na mpango mkakati wa miundombinu ili kukuza na kuongeza jitihada za kushughulisha mwili hasa shuleni

Hatua madhubuti za sera kudhibiti uingiliaji wa viwanda katika michakato ya utengenezaji wa sera za umma

Kuimarisha sekta mbalimbali kwa ajili ya kuratibu magonjwa yasiyoambukiza ili kuongeza upatikanaji wa rasilimali ikiwemo fedha za kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza.

Kuongeza bajeti ya taifa iliyoelekezwa katika kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza

Matibabu, Matunzo Na Msaada



MUHTASARI

Sisi, watu tunaishi na magonjwa yasiyoambukiza tunaishi na hali sugu na ulemavu ambao unahitaji matibabu ya mara kwa mara ambayo husababisha gharama kubwa ya kifedha kwa familia zetu.

Tunastahili kuungwa mkono na taasisi za serikali, watoa huduma za afya na familia. Wakati wa janga la UVIKO-19 tuliteseka sana kwani tuko katika hatari kubwa ya kuambukizwa na virusi, ilikuwa ngumu kufikia vituo vya matibabu na watoa huduma za afya hawakuwa wakitupa taarifa za kutosha na msaada ili kujikimu wakati wa janga hilo.

Tunaiomba serikali kuimarisha mifumo ya afya na kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya ili kusaidia watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza, ikiwa ni pamoja na wakati wa magonjwa ya milipuko kwa siku zijazo. Tunahitaji maelezo zaidi kuhusu hali zetu ili kujizidhibiti vyema, kuhakikisha ufuatiliaji wa matibabu, na kuhakikisha tunajiboresha kiafya.

Katika vituo vingi watoa huduma za afya bado hawajafunzwa kuhusu magonjwa yasiyoambukiza ili kutoa elimu ifaayo juu ya usimamizi wa hali zetu, hasa kuhusu masuala ya lishe.

Watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza wanakabiliwa na matumizi makubwa ya fedha kwa sababu ya ukosefu wa bima. Tunahitaji upatikanaji rahisi wa bima, ambayo pia ni nafuu. Gharama kubwa zinazohusiana na matibabu na matunzo yatokanayo na magonjwa yasiyoambukiza zimesababisha watu wengi wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza kupoteza biashara na mapato yao.

Sisi, tunaishi na magonjwa yasiyoyakuambukiza, tunaomba:

Upatikanaji wa huduma za afya ili kuwezesha uchunguzi wa awali, utambuzi na matibabu ya mapema, kutoa huduma za kisaikolojia na kuboresha maisha kwa wale wenye magonjwa yasiyoambukiza.

Kuimarisha vituo vya huduma za afya katika ngazi za msingi ili kuhakikisha upatikanaji nafuu wa dawa muhimu, kupunguza umbali, gharama za matibabu na kuwezesha upatikanaji wa huduma stahiki kwa wakati.

Serikali ihakikishe bima za afya na mahitaji yote muhimu (dawa na vipimo) kwa watu waishio na magonjwa yasiyoambukiza.

Kuhakikisha Mafunzo ya ubora na ya kitaalamu juu ya magonjwa yasiyoambukiza kwa watoa huduma za afya katika ngazi zote

Mafunzo, ushauri nasaha na msaada kwa watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza na ulemavu utokanao na magonjwa yasiyoambukiza juu ya kujimudu

Kutambua jukumu la wanafamilia, walezi na wasaidizi kuwa na nguvu kubwa ya uponyaji katika kusaidia watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza.

Kuandaa na kuwasilisha taarifa zinazofanana juu ya maswala ya lishe kwa watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza.

Kutengeneza na kuhakikisha upatikanaji wa pasipoti ya afya kwa watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza kuwezesha ufuatiliaji wa matibabu.



Tupo imara



Sisi tuna ujuzi na uzoefu na tunaweza kusimamia hali zetu za kiafya



Sisi ni watu ambao tuna:
- Haki
- Mahitaji
- Matumaini
- Wajibu
- Matarajio



Meaningful Involvement



MUHTASARI

Sisi, tunaishi na magonjwa yasiyoyakuambukiza tuna uwezo na hatupaswi kuachwa nyuma katika maamuzi ambayo yanahusu afya na hali zetu, huenda tusiwe na ujuzi wa kiufundi kila wakati, lakini uzoefu wetu wa maisha unaweza kutoa taswira halisi na muhimu kushughulikia changamoto za maisha zinazosababishwa na magonjwa yasiyo yakuambukiza. Sisi ni shuhuda hai za hali zetu. Tunaweza kusaidia wapanga mipango na watunga sera kuelewa mahitaji yetu na kujibu sera na programu zinazofaa za afya.

Kwa hiyo, tunatoa wito kuwe na mipango ya kuwashirikisha watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza katika michakato ya kufanya maamuzi yanayohusiana na Magonjwa yasiyoyakuambukiza. Ushiriki wetu unahitaji kuwa wa kina na tunapaswa kuchukuliwa kama washirika sawa na wengine. Tunahitaji kuunganishwa na serikali, washikadau na jamii ili ushiriki wa kikamilifu ufanyike na tuweze kuwasilisha uzoefu wetu wenyewe na kupambana na unyanyapaa na ubaguzi unaohusiana na Magonjwa yasiyoyakuambukiza .

Tunataka kutambuliwa kama watu wenye haki, mahitaji, matumaini, wajibu na matarajio. Tuko tayari kushiriki uzoefu wetu wa maisha na kuleta mabadiliko lakini pia tunaomba kutoa wito na kuwa na mazingira wezeshi ambayo yanakuza ushiriki wetu wa vitendo na kutupa fursa ya kuzungumza.

Kama watu tunaishi na Magonjwa yasiyoambukiza , tunaomba kuhusika katika utungaji sera na michakato ya uwajibikaji, kusaidia kuunda na kufuatilia programu na huduma zinazoathiri maisha yetu ya kila siku, kuchukua jukumu tendaji katika utawala na kuwa mstari wa mbele katika utetezi wa magonjwa yasiyoyakuambukiza.

Sisi, tunaishi na magonjwa yasiyoyakuambukiza, tunaomba:

Mafunzo, ushauri na msaada ili kuboresha maarifa na ujuzi wetu, na kuimarisha ushiriki mzuri wa watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza katika michakato ya uhamasishaji wa afya, utengenezaji wa sera na juhudi za utetezi.

Kusaidiwa katika kuanzisha na kuimarisha ushirikiano na serikali na wadau wengine ikiwemo jamii, ili kukuza na kuongeza shughuli zinazofanywa na kuongozwa na watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza


Kupata taarifa kwa wakati juu ya magonjwa, visababishi, njia za kuzuia na kutibu, ili kuimarisha maarifa na ujuzi wetu

Kukuza na kuimarisha asasi za kiraia na uanzishaji wa vikundi vya watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza ambao ni wasemaji wakuu wa mahitaji ya wagonjwa.

Ushirikishwaji wa watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza katika hatua za uundaji.

**"Sisi ni sauti ya wale
wasioweza kupaza sauti"**

#NCDvoices





MAONI YETU, SAUTI YETU

An initiative by the NCD Alliance and people living with NCDs



Ili kujifunza zaidi kuhusu Ajenda ya Kimataifa ya Utetezi ya Watu Wanaoishi na Magonjwa yasiyoambukiza tembelea:

ourviewsourvoices.org

[#NCDvoices](https://twitter.com/NCDvoices)